TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo,
Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam
"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Kumb na: Taro /P/2022/ A09 **: Swahili Version:** Tarehe: 20 Machi 2022

# MAONI KUHUSU MJADALA UNAOENDELEA WA UTEUZI WA MSEMAJI MKUU WA SHIRIKISHO LA MUZIKI TANZANIA

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** ambapo kwa lugha ya Kiswahili linajulikana kama **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Mnamo tarehe 16 Machi 2022, baadhi ya viongozi wa Shirikisho la Muziki Tanzania waliitisha mkutano wa waandishi wa habari na kuutangazia umma juu ya uteuzi wa Bw.Steve Mengele (Steve Nyerere) kuwa Msemaji Mkuu wa Shirikisho la Muziki Tanzania. Mkutano huo ulionekana kuendeshwa na Raisi wa Shirikisho la Muziki (Wakili Addo Novemba), Makamu (Mzee Yusuph) na Katibu Mkuu (Fareed Kubanda). Kitendo hicho kilishuhudiwa na kutokuungwa mkono na wadau mbalimbali wa muziki Tanzania na kusababisha mjadala mkubwa wenye hisia kali miongoni mwa wasanii na wadau wake.

Mnamo tarehe 18 Machi 2022, Shirikisho la Muziki Tanzania kupitia Katibu Mkuu wake, lilitoa taarifa na wito kwa wadau wa muziki, viongozi wa vyama vya muziki na wasanii kushiriki **kikao** cha dharura kitakachofanyika tarehe 21 Machi 2022, Jangwani Sea Breeze Resort. **Kikao** hicho kimekusudiwa kujadili uteuzi wa Nafasi ya MSEMAJI MKUU wa Shirikisho.

Mnamo tarehe 18 Machi 2022, Gazeti la Mwanachi, lilichapisha mahojiano na Katibu Uenezi wa Shirikisho la Muziki Tanzania (Bw. Siza Mazongera) na alisikika akisema ***"Mimi ndio Msemaji Shirikisho kwa mujibu wa katiba yetu, kwasababu nilichaguliwa kwenye uchaguzi uliofanyika Aprili 2021 baada ya kugombea na kushinda asilimia 80"***

**HOJA ZA KISHERIA**

**Je nafasi ya Msemaji Mkuu ni nafasi halali kisheria katika Shirikisho la Muziki Tanzania?**

A. Kwa mujibu wa kifungu cha **7.1.3** cha Katiba ya **Shirikisho la Muziki Tanzania** kimempa raisi wa Shirikisho jukumu la kuwa msemaji mkuu wa Shirikisho la Muziki Tanzania
B. Kwa mujibu wa kifungu cha **7.3.9** cha Katiba ya **Shirikisho la Muziki Tanzania** kimempa Katibu Mkuu wa Shirikisho jukumu la kuwa msemaji mkuu wa shughuli za siku hadi siku za Shirikisho la Muziki Tanzania.

**Je kuna uhalali wa kisheria kwa Shirikisho la Muziki Tanzania kuitisha kikao cha kufanya maamuzi ya Shirikisho kwa kuwahusisha moja kwa moja watu wa nje ya shirikisho (wadau na wanachama wa vyama vya muziki)?**

A. Kwa mujibu wa vifungu vya 3.1, 6.1, 6.2, 6.3 ,6.2.7 vya Katiba ya **Shirikisho la Muziki Tanzania** vinaelekeza kuwa maamuzi ya shirikisho yanaweza kufanywa na Mkutano Mkuu ikiwa ndiyo chombo cha juu, Bodi ya Shirikisho na Sekretariati tu.
B. Kwa mujibu wa vifungu vya **5.1.1** na **5.1.2** vya Katiba ya **Shirikisho la Muziki Tanzania** vinaelekeza kuwa wanachama wa shirikisho watakua vyama vya muziki.
*C.* Kwa mujibu wa kanuni **21(3)** ya **Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa Mwaka 2018** inaelekeza kuwa *"Chama cha Sanaa kitakua sehemu ya Shirikisho kulingana na fani ama kazi ya sanaa husika kwa mujibu wa taratibu kitakachojiwekea kwa misingi ya katiba yake"*

**HITIMISHO**

Kwa mujibu wa Katiba ya Shirikisho la Muziki Tanzania, nafasi ya MSEMAJI MKUU WA SHIRIKISHO haipo bali kuna majukumu ya viongozi wa Shirikisho kuwa wasemaji wakuu wa Shirikisho. **HIVYO BASI**, Kitendo cha baadhi ya viongozi wa Shirikisho kumteua Bw. Steve Mengele (Steve Nyerere) kuwa Msemaji Mkuu wa Shirikisho la Muziki Tanzania ni batili na hakina mashiko kwa mujibu wa Katiba ya **Shirikisho la Muziki Tanzania,** kwasababu nafasi hiyo haipo katika katiba ya Shirikisho. Shirikisho lilipaswa kuitisha mkutano Mkuu na kuifanyia marekebisho katiba yao ili kuongeza nafasi hiyo kabla ya kufanya maamuzi ya uteuzi huo.

Kutokana na ukweli kwamba nafasi ya MSEMAJI MKUU WA SHRIKISHO haipo kwa mujibu wa katiba ya Shirikisho la Muziki Tanzania, kuweka kikao chochote na kujadili uteuzi wa mtu kwenye nafasi hiyo (isiyokuwepo) ni kitendo batili kwa sababu kinakiuka Katiba ya **Shirikisho la Muziki Tanzania**

Kwa mujibu wa Katiba ya Shirikisho la Muziki Tanzania na Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa, wadau wa muziki na wanachama wa vyama vya muziki hawana nafasi ya kushiriki moja kwa moja katika kufanya maamuzi ya Shirikisho la Muziki Tanzania, bali wanaweza kushiriki kupitia viongozi wao wa vyama ambao ni wajumbe katika Mkutano Mkuu wa Shirikisho, Bodi ya Shirikisho na Sekritarieti. Hivyo basi kikao kilichopangwa na Katibu Mkuu wa Shirikisho la

Muziki Tanzania, kuwashirikisha wadau na wasanii moja kwa moja katika kujadili uteuzi wa Msemaji Mkuu wa Shirikisho (Tarehe 21 Machi 2022, Jangwani Sea Breeze Resort) ni batili na hakina mashiko kisheria katika kufanya maamuzi ya Shirikisho la Muziki Tanzania.

TARO tunalishauri **Shirikisho la Muziki Tanzania,** kuacha kuendelea na shughuli na mienendo inayovunja katiba ya Shirikisho, na badala yake watafute kwanza ushauri wa kisheria utakaowaongoza kukabiliana na changamoto iliyopo, ambayo inahitaji kutatuliwa kitaalamu kuepusha migogoro zaidi na kulinda heshima na hadhi ya Shirikisho la Muziki Tanzania.

TARO kama taasisi iliyosajiliwa kusaidia wasanii tuko tayari kutoa ushauri ili kudumisha heshima na hadhi ya shirikisho.

ASANTENI
MUNGU AIBARIKI TANZANIA
MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA
(Kazi iendelee)

Wako katika kujenga Taifa

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**

TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION